

# Msumbiji yatilia mkazo ulinzi wa mgambo

U. 1-3-88

Na Mwandishi Wetu

**MJUMBE wa Kamati Kuu ya Chama kinachotawala nchini Msumbiji (FRELIMO)** Ndugu Oscar Monteiro amesema kuwa Msumbiji sasa inajimarisha zaidi mpango wa ulinzi wa mgambo wa wananchi kujilinda wenyewe ikiwani njia mojawapo ya kukabiliana na magaidi wa MNR.

Akizungumza na wanachama wa Chama cha Mshikamano kati ya Tanzania na Msumbiji (Tamosa) mjini Dar es Salaam jana, alisema kuwa katika mapambano kama haya jeshi peke yake halitoshi, bali vilevile ni kuwaandaa wananchi vijijini katika ulinzi wa mgambo.

Magaidi wanaosaidiwa na utawala wa Makaburu wa Afrika Kusini wanachofanya hivi sasa ni kujaribu kuhujumu uchumi wa nchi ili kurudisha

maendeleo ya nchi nyuma kwa kuharibu shule, hospitali na maeneo mengine ya kuendeleza uchumi, alisema.

Mjumbe huyu wa Kamati Kuu ya Frelimo, pia ni Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Tawala za Mikoa, alikuwa akielezea hali ilivyo nchini Msumbiji.

Alisema kuwa magaidi hivi sasa wanatumia nguvu kwa kuwalazimisha

wananchi wajunge nao na wamegundua mbinu mpya ya kuwahadaa watoto wenyewe umri kati ya miaka tisa na kumi kwa kuwapatia vitu vya kuwasurahisha kama chakula cha kutosha na baadaye kuwalazimisha kufanya mashambulizi.

Ndugu Monteiro, ambaye amekuwa katika ziara ya wiki mbili ya Tanzania alieleza kuwa magaidi wametumia hali ngumu inayoikabili Msumbiji kutohana na ukame ulioikumba kwa muda wa miaka sita sasa kujiiamarisha.

Hata hivyo, alisema, njia pekee ya kukabiliana na magaidi ni kuendelea kufanya kazi kwa bidii kwani nia yao ni kutaka kuona uchumi unadidimia kabisa.

Akizungumzia kuhusu Tamofa wenyewe, alisema kuwa itazidi kuimarisha mashikamano uliokuwepo kati ya wananchi wa Tanzania na Msumbiji dhidi ya maadui wa nchi bizi mbili.

Alisema kuwa Tamofa ina jukumu la kuwaelimisha wananchi wa pande zote mbili hali ilivyo nchini Msumbiji.

Naye Mwenyekiti wa Tamofa ambaye ni Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Ndugu Charles Kilco, alisema, Tanzania iko tayari, kuśaidiana na wananchi wa Msumbiji katika kukabiliana na magaidi.

Msumbiji  
magaidi  
mwele  
militaris